



Chukua katika mali yake kwa wema, kiasi kinachokutosha wewe na wanao

Imepokelewa kutoka kwa Aisha mama wa waumini radhi za Allah ziwe juu yake amesema: Aliingia Hindu binti Utba mke wa Abuu Sufiani kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, akasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hakika Abuu Sufiani ni mwanaume bahili sana, hanipi matumizi yanayonitoshia mimi na wanangu isipokuwa kiasi ninachokichukua katika mali yake pasina yeye kujua, je kwa hilo nina tatizo? Akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: "Chukua katika mali yake kwa wema, kiasi kinachokutosha wewe na wanao".

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Alitaka kujua Hindu binti Utba radhi za Allah ziwe juu yake kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuhusu mume wake Abuu Sufiani radhi za Allah ziwe juu yake, na kwamba yeye ni mwanaume bahili mwenye pupa sana na mali yake, hampi katika matumizi kiasi kinachomtoshia yeye na wanaye, mpaka achukue katika mali yake kwa siri hali yakuwa hajui, je ana dhambi juu yake katika hilo?. Akasema rehema na amani ziwe juu yake: Chukua kwa ajili yako na watoto wako katika mali yake kiasi kinachojulikana katika mazingira ya kawaida na kwamba hicho ndicho kitakachomtoshela hata asipojua.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/2965>

